

Chanjo ya lazima kwa mifugo yaja

Na Gwamaka Allipili

SERIKALI inatarajia kuanzisha utaratibu wa kutoa chanjo ya lazima kwa mifugo kila baada ya miezi mitatu lengo likiwa kuzuia magonjwa kwa mifugo, binadamu na kuipa thamani nyama ya Tanzania katika masoko ya kimataifa.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema hayo jana Ikulu, jijini Dar es Salaam, wakati wa mkutano na waandishi wa habari uliolenga kutoa mrejesho wa ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoifanya Morocco na Saudi Arabia hivi karibuni.

Ulega alisema hivi sasa kuna tatizo kubwa la mifugo nchini kushambuliwa na magonjwa yanayosababisha athari mbalimbali vikiwamo vifo, magonjwa kwa binadamu pindi anapokula nyama yenye vimelea vya wadudu na nyama kutokukidhi ubora katika masoko ya kimataifa.

Alisema kutokana na hali hiyo, wizara inatarajia kuanzisha kampeni ya kuchanja mifugo kwa lazima kwa utaratibu maalum na kampeni hiyo itazinduliwa na Rais Samia. Mbali na kampeni hiyo, alisema Rais Samia pia atazindua kiwanda kitakachotengeneza chanjo hizo.

"Utawekwa utaratibu maalum wa kuchanja, kama ni kila baada ya miezi mitatu, kwamba kila mfugaji atalazimika kuchanja mifugo yake. Tunataka tuuze kwa wingi nyama katika soko la kimataifa, pamoja na kuzuia magonjwa yatokanayo na kula nyama yenye virusi," alisema Ulega.

Ulega alisema mwaka 2021 Tanzania iliua nyama tani 1,700 katika soko la dunia na hadi sasa tani

14,000 zimeshauzwa kiasi ambacho ni kidogo.

Alisema hadi Juni, mwaka huu Saudi Arabia ilinunua tani 1,400 za nyama kutoka Tanzania huku mahitaji yao yakiwa ni tani 21,000.

"Bado tunafuga kizamani, tunafuga kimila. Tunatakiwa tufuge kibiashara, tunatakiwa tupeleke mifugo sokoni. Ni kweli mifugo ni utajiri lakini ni lazima ifike sokoni," alisema Ulega.

Mkurugenzi wa Mashariki ya Kati kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Abdallah Kilima, aliwasili Watanzania wanaokwenda kufanya kazi katika nchi za Mashariki ya Kati wafuate utaratibu ili wawe salama.

Alisema nchi za Mashariki ya Kati zinategemea nguvu kazi kutoka kwa wageni wanaofika kufanya kazi.

Balozi Kilima alitolea mfano akisema Oman ina idadi ya watu milioni tano lakini watu milioni

2.4 ni wageni. Kati ya wageni hao, kutoka India ni 800,000 na Wapakistan ni 300,000. Pia alisema Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) asilimia 60 ya wakazi wake ni wageni.

Alisema asilimia 92 ya taarifa kwamba wageni wanateswa katika nchi za Mashariki ya Kati si kweli, akitolea mfano kwamba kuna Watanzania 25,000 Oman kati yao 17,000 wanafanya kazi za ndani.

"Wafanyakazi wa ndani Oman kima cha chini wanalipwa Dola za Marekani 300 kwa mwezi. Wako Watanzania wanaohudumia familia zao huku Tanzania kwa kazi wanazofanya Oman. Ukifuata utaratibu hutapata matatizo," alisema.

Mkurugenzi wa Uhamasishaji Uwekezaji kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), John Mathew, alisema kuanzia Julai hadi Septemba, mwaka huu, TIC imeandikisha miradi 137 na kutengeneza ajira 86,900.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 28 2324455
Fax: +255 28 2323233
Barua Pepe: @mow.go.tz
Tovuti: www.mwte.go.tz



Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
16.11.2023

TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumamosi tarehe 18-11-2023 hadi 20-11-2023 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero kupitia Mikumi, gari hizo zina namba za usajili: **T 289 EDD / T 879 EAU T 204 DYJ / T 881 EAU T 203 DYJ / T 568 EAZ**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

Urefu - mita 20.00
Upana - mita 4.20
Kimo - mita 5.40

2. Njia itakayotumika: Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi, gari zitafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.



Majaliwa aagiza wanaolisha mifugo mashambani wachukuliwe hatua

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Namilema, alipokuwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo katika Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi, jana. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)

>>UK.3



Biashara wa UPL,
Alex Kanyambo.
(Picha na
Christopher Lissa).

kwa wanafunzi wa Tanzania.

Katika kuimarisha uhusiano huo, mwaka 2018 Tanzania na Romania zilitia saini hati ya makubaliano kuhusu ushauriano wa kisiasa na kidiplomasia.

UHURU UK 3

* Majaliwa aagiza wanaolisha mifugo mashambani wachukuliwe hatua *

Na MWANDISHI MAALUMU, Lindi

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemwagiza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, ahakikishe wafugaji walioingiza mifugo katika mashamba na kusababisha uharibifu wa mazao, wakamatwe na kufikishwa mahakamani kwani hakuna yeyote ambaye yuko juu ya sheria.

Majaliwa alitoa agizo hilo wilayani Ruangwa mkoani Lindi, jana alipozungumza na wananchi katika vijiji vya Namkatila, Matambarale na Nandandala akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa.

Alisema vijiji hivyo ni miongoni mwa maeneo yaliyoathirika zaidi na migogoro ya wakulima na wafugaji ikiwemo mkulima mmoja kuuawa.

"Serikali iko macho na itamchukulia hatua yeyote anayeathiri shughuli za wengine, Tanzania ni nchi inayoendeshwa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu, hivyo watendaji wote wa vijiji wawajibike kwa kutekeleza majukumu

yao ipasavyo kuepusha migogoro isiyo na tija. Tutaendelea kuwalinda wananchi," alisema.

Waziri Mkuu alisema serikali haitovumilia kuona jamii ya wafugaji wasiozingatia sheria na haitatoa nafasi kwa wakulima kuendelea kuharibiwa mazao yao.

"Jambo hili halikubaliki na hatua kali zitachukuliwa kwa watu wote wanaotaka kuvuruga amani, serikali haitavumilia vitendo hivyo... Hatutamsamehe mfugaji anayetumia fimbo yake kumpiga mkulima baada ya kulisha mifugo katika shamba lake.

"Hatuna nafasi ya kushuhudia hayo, utaratibu lazima uzingatiwe, tukomeshe migogoro ya wafugaji na wakulima. Tumuache mkulima aendelee kulima avune. Tusilinde waovu," alisema.

Majaliwa alisema kauli ya serikali ya kuthamini shughuli za kilimo na ufugaji nchini haimaanishi wafugaji wanaruhusiwa kuingiza mifugo na kulisha katika mashamba ya

wakulima, wala wakulima kudhuru mifugo ya wafugaji.

Alisisitiza wafanye shughuli zao kwa kuzingatia sheria na taratibu, kwani tayari serikali imeshaandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa kutenga maeneo ya makazi, huduma za kijamii, kilimo na mifugo hivyo hakuna mwenye haki ya kumvamia mwingine.

Majaliwa alieleza watendaji wa vijiji wahakikishe kabla ya kuwakaribisha wafugaji katika maeneo yao wajiridhishe kama wana maeneo ya kutosha kwa shughuli hiyo na kuwashirikisha wanakijiji husika juu ya ujio wa wafugaji na wafahamu idadi ya mifugo waliyonayo.

"Wananchi tulieni mkiona maeneo yenu yamevamiwa toeni taarifa. Hapa tusisikie tena athari hizi," alisema.

Alitumia fursa hiyo kuwataka wananchi hao waendeleo na shughuli za kilimo na

wasiogopewa, kwani serikali ipo makini na inaendelea kuimarisha ulinzi katika maeneo yote.

Hata hivyo, wananchi hao walimweleza Waziri Mkuu Majaliwa wanaogopa kuandaa mashamba kutokana na kuhofia uvamizi wa mifugo.

Katika hatua nyingine, Majaliwa alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alisisitiza wananchi lazima wafikishiwe huduma za kijamii karibu na makazi, hivyo kwa kushirikiana na watendaji wengine wa serikali atahakikisha miradi ya maendeleo inasimiwa na kutekelezwa ipasavyo ikiwemo kukamilika kwa wakati na viwango kusudiwa.

Pia, Majaliwa alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Frank Chonya, kukamilisha ujenzi wa zahanati ya Kijiji cha Namilema, baada ya wananchi kumwomba awasaidie kuimalizia kutokana na kujenga boma kwa nguvu zao.

* Ulega: Rais Samia ametangaza fursa lukuki mifugo, uvuvi

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amesema Rais Samia Sulu-hu Hassan amefanya kazi kubwa kutangaza fursa na kutafuta masoko katika sekta za mifugo na uvuvi.

Ulega amesema kazi alizofanya Rais Samia nchini Saudi Arabia imewezesha nchi kupata soko la nyama kuanza uzalishaji wa majani ya kulisha mifugo.

Ulega alisema hayo Ikulu Dar es Salaam jana kwenye mkutano wa waandishi wa habari ulioandaliwa na Kuru-genzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu kuzungumzia ziara ya Rais Samia nchini Morocco na Saudi Arabia Novemba 8 hadi 11, mwaka huu.

Alisema mwaka 2021 Tanzania iliua tani 1,700

za nyama nje ya nchi lakini mpaka sasa imeuza zaidi ya tani 14,000.

"Haya mambo hayaji kimsihara ni kutokana na jitihada na mikakati na ni kutokana na matokeo ya ziara ambazo Rais Samia amezifanya ili kuongeza zaidi biashara na kuvutia wawekezaji," alisema Ulega.

Alisema Saudi Arabia pekee ambao awali hawakuwa wakichukua nyama kutoka Tanzania mpaka Juni mwaka huu wamenunua tani 1,400 na mahitaji yao ni tani 20,000 kwa mwezi.

"Mifugo ni utajiri hivyo ni lazima tutangulize kwanza biashara yaani kila anayefuga afuge kwa malengo ya kupata fedha. Kila baada ya muda tunavuna na kupeleka sokoni ili kuweza kufaidika. Kwani hata tani hizi 14,000 tulizozuia asilimia 80 ni mbuzi na kon-

doo kwa upande wa ng'ombe bado hatujafanikiwa," alisema Ulega.

Alisema serikali imekua ikifanya mbinu kuongeza uzalishaji wa ng'ombe wanaokidhi vigezo vya soko la nje ya nchi.

Alivitaka vyama vya ushirika vya wafugaji kuhamasisha wafugaji wavune mifugo yao na kutajirika na isiwe fahari kuwa na ng'ombe 1,000 mpaka 2,000 huku mifugo hiyo ikiwa haiendi sokoni.

Ulega alitaja mikakati ya kuongeza uzalishaji wa nyama kuwa ni kupitia upandikizaji wa mbegu bora na kupitia Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kwa kuifanya kuwa kampuni mama ya biashara ya nyama na pia kupitia programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT).

"Kwenye BBT tutatumia vijana ambao ni wafanyabi-

ashara wa mitugo kila mmoja kupitia vikundi vyao ana akaunti benki kwa ajili ya kuwezesha. Tunataka hawa wanaotaka nyama wananenepeshewa moja kwa moja kupitia hawa vijana ambao tunawapa vitalu wazalishe na kuuza kulingana na mahitaji," alisema.

Aliongeza: "Tuna mifugo mingi sana ila changamoto inakua mtu anapohitaji inakua shida kuipata na ni kwa sababu wafugaji wako scattered hivyo tunachokifanya ni kustreamline ili wenye kuhitaji kununua wasipate tabu."

Pia, kupitia mkutano huo, Ulega alitangaza mpango wa serikali kuanzisha kampeni ya kila mfugaji nchini lazima mifugo yake ichanjwe ili kuondoa magonjwa ya mifugo yanayoweza kuleta changamoto kwenye soko la mifugo.

Mangapwa za moja kw 1,000 zisizo Alisema sasa Banda 98.

Dk Mk za Mareka binu ya m barabara, eneo hilo yatakayo Pia, al

kuingiza kwa ajili gharama

Mku alisema nchi im jumuis na kich 200,000.

Zuh la Man ya Mali

Aid zaidi y wa bar wa ma ya bar magha

Ali uletaji kuwa yaani kuwa wa E B nye i

Dar plans livestock mass vaccination

By HILDA MHAGAMA

TANZANIA intends to undertake a nationwide livestock mass vaccination campaign to increase the livestock export market and farmers' revenues.

Livestock and Fisheries Minister Abdallah Ulega disclosed this yesterday at the State House in Dar es Salaam during a news conference on President Samia Suluhu Hassan's trips to Morocco and Saudi Arabia, held between November 8 and 11 this year.

Mr Ulega stated that one of the challenges facing Tanzanian livestock in meeting export requirements was pests and diseases, and the campaign was one of the measures employed by the government to shift the narrative.

"At present, they vaccinate, but everyone does it according to their schedule. We want every livestock keeper to vaccinate, and we will de-



MR Ulega

velop a specific vaccination schedule for each livestock disease," he stated.

He asserted that the campaign would contribute to increasing confidence in Tanzania's meat standards and quality among the nations with whom Tanzania conducts interna-

"At present, they vaccinate, but everyone does it according to their schedule. We want every livestock keeper to vaccinate, and we will develop a specific vaccination schedule for each livestock disease."

tional business.

In order to continue fostering confidence among overseas purchasers, the government has also set aside disease-free compartment zones.

Mr Ulega said that during their visit to Saudi Arabia, they had meetings with the Almarai company, which is ready to come to Tanzania and start a project to produce livestock fodder. The company has already started negotiations with the Ministry of Livestock to initiate the project.

Continues on Page 3

... signed an Agreement on Political and Diplomatic Consultations.

Additionally, both leaders will witness the signing

implementing economic diplomacy.

Dar plans livestock mass vaccination

Continued from Page 1

Other companies that showed interest include the Salic Company and the Crown Agricultural Company, both of which aim to start projects for the cultivation of livestock feed (alfalfa) and a project to fatten cows for sale in the Middle East market.

"Those companies have also requested to start cooperative associations of farmers who will cultivate alfalfa livestock feed, and they will establish joint collection centres for the companies," said Mr Ulega.

He stated that Tanzania has the largest livestock population, but the problem is that when someone wants to buy, it is difficult to find since the herders are dispersed.

"So, what we are doing is streamlining the process so that those who need to buy do not have trouble," he said.

According to the minister, the deal they have with these firms is to perform contract farming. The farmers will be given seeds, and after harvesting, there will be collection centres.

"In 2021, we sold 1,700 tonnes of meat abroad, but until now, we have sold more than 14,000 tonnes. This is due to the results of the visits that President Samia has made to increase business

and attract investors," he told reporters.

According to the minister, Saudi Arabia, which did not buy meat from Tanzania until June of this year, has already purchased 1,400 tonnes, and their need is 20,000 tonnes in one month, so the opportunity is still quite large.

"The Saudis are ready to cooperate with Tanzania, and the first step is to ensure that we have out growers to be able to reach the Saudi market effectively," stated Mr Ulega.

As a government, he said they have been implementing various methods to increase the production of cows that meet the criteria of the foreign market, including artificial insemination.

In September of this year, when speaking at the Africa Food System Forum 2023 in Dar es Salaam, Minister Ulega outlined some of the interventions and opportunities focused on boosting commercial livestock production to increase the supply of raw materials for processing industries.

These interventions include the implementation of the Livestock Sector Transformation Plan (LSTP), which includes improving animal breeds through artificial insemination and the use of improved breeding bulls,

strengthening pasture and water development by establishing commercial farms for pasture and pasture seed production.

He mentioned other initiatives such as strengthening animal health systems through vaccination campaigns and control of ticks and tick-borne diseases, enhancing extension services by equipping extension officers with extension kits and transportation, research, and training.

The list of initiatives also includes the value addition of livestock products, creating an enabling environment for business and investment, and mainstreaming employment opportunities through the engagement of youth and women under the auspices of Building a Better Tomorrow through Livestock and Fisheries Entrepreneurs (BBT-LIFE).

"We have recruited 240 youth in the BBT-LIFE programme, whereby the beneficiaries have been acquainted with the necessary innovative mind transformation, entrepreneurship skills, and business-oriented perspectives. They are expected to significantly contribute to increased production, value addition, and employment inclusion," he stated.